



# MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR

## TAARIFA KWA UMMA

### ULAZIMA WA HATI YA UTHIBITISHO WA KULIPA KODI (TAX CLEARANCE CERTIFICATE)

Zanzibar, 09 Mei, 2023:

#### 1. UTANGULIZI:

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inaziarifu mamlaka zote zinazotoa leseni ndani ya Zanzibar kutekeleza wajibu wao wa kisheria wa **KUTOTOA** Leseni yoyote ya biashara katika maombi yasiyokuwa na **HATI YA UTHIBITISHO WA KULIPA KODI** kama inavyoelezwa chini ya **kifungu cha 16 (2) cha Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi, Nambari 7, ya 2009**. Kifungu cha Sheria husika, kimekusudia Mamlaka ya Leseni kuwa ni pamoja na Wizara za Serikali, Taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA) zenye jukumu la kutoa leseni, cheti cha kufanya kazi au nyaraka zozote halali ambazo hulazimika kutolewa kila wakati kwa mujibu wa Sheria za Mamlaka husika.

#### 2. MAHITAJI YA SHERIA:

Maombi yote ya leseni ya biashara, na nyaraka zinazofanana kwa ajili ya idhini yoyote kutoka mamlaka yoyote ya leseni au vibali yataambatanishwa na **HATI YA UTHIBITISHO WA KULIPAKODI** kutoka kwa **Kamishna Mkuu** wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kama ilivyoelezwa chini ya **kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi, Nambari 7, ya 2009**, kupitia taratibu zifuatazo:

- 2.1 Waombaji wa leseni wanatakiwa kuomba Hati ya Uthibitisho wa Kulipa Kodi kwa Kamishna Mkuu wa ZRA kupitia ofisi yoyote ya ZRA Unguja na Pemba, kwa kujaza Fomu **Namba. 410 TC**.
- 2.2 Maombi yatafanyiwa kazi kwa haraka na Hati ya Uthibitisho wa Kulipa Kodi itatolewa mara moja.
- 2.3 Hati ya Uthibitisho wa Kulipa Kodi itawasilishwa kwa Mamlaka ya utoaji Leseni husika.
- 2.4 Mamlaka ya utoaji leseni husika itatoa leseni baada ya kupokea Hati ya Uthibitisho wa Kulipa Kodi iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar.

#### 3. MATOKEO YA KUTOKUFUATA SHERIA:


Mtu yeyote ambaye anatoa leseni yoyote ya biashara bila ya **HATI YA UTHIBITISHO WA KULIPAKODI** iliyotolewa na ZRA na kuchangia upotevu wa mapato ya Serikali, atakuwa ametenda kosa na ataadhibiwa kwa mujibu wa **kifungu cha 55 cha Sheria ya Usimamizi na Taratibu za Kodi namba 7 ya mwaka 2009**.

#### 4. HITIMISHO:

ZRA inazitaka Mamlaka zote za Leseni kutekeleza wajibu wao wa kisheria wa **KUTOTOA** Leseni ya biashara kwa waombaji bila ya **HATI YA UTHIBITISHO WA KULIPAKODI** kutoka ZRA ili kuepuka kuisababishia hasara ya mapato Serikali na kutenda kosa. ZRA, itasimamia uwajibikaji wa hitaji hili la kisheria kwa kuzifanyia ukaguzi wa kikodi taasisi hizo ili kuhamasisha utekelezaji wa Sheria.

**"Tulipe Kodi kwa Maendeleo ya Zanzibar"**

Imetolewa na:

  
Yusuph Juma Mwenda  
Kamishna Mkuu